ewura

Energy and Water Utilities Regulatory Authority

NEWSLETTER

SEPTEMBA 2009

ISSN I821-7273 ISSUE NO.002

- Hongera, Wabunge waipongeza EWURA
- Changamoto katika utoaji leseni za biashara ya mafuta
- Uteuzi
- Kuelekea kwenye ununuzi wa mafuta kwa pamoja

YALIYOMO

Kutoka kwa Mhariri	4
Kutoka Dawati la Mkurugenzi Mkuu	5
Kuelekea kwenye ununuzi wa mafuta kwa pamoja	6
EWURA yapambana na VVU/UKIMWI	7
DAWASA yapewa muda kuboresha huduma zake	8
Uteuzi	9
EWURA yaendesha mafunzo kwa mamlaka za maji	10
Kubadilishana uzoefu na kuanzisha ushirikiano kuhusu mbinu bora za udhibiti ni lazima	11
Changamoto katika utoaji leseni za biashara ya mafuta	13
Matukio katika picha	14
EWURA yapiga hatua katika kumlinda mlaji	16
Hongera, Wabunge waipongeza EWURA	18
Kampeni ya EWURA ya uhamasishaji yaingia Songea na Tunduru kwa kishindo	20
Marekebisho katika kuinua maendeleo ya miradi Midogo ya nishati Tanzania	21
Maadhimisho ya miaka mitatu ya EWURA	23

BODI YA WAHARIRI

MWENYEKITI

Bw. Haruna Masebu

MHARIRI

Bw. Titus Kaguo

WAJUMBE

Bi Muna Mahanyu

Bw. Felix Ngamlagosi

Mhandisi Charles Omujuni

SEKRETARIATI

Bi. Amina Shamte

Bi. Janet Mwaipopo

Ofisi ya EWURA

Ghorofa ya Sita,

Harbour View Towers,

Barabara ya Samora

S.L.P 72175,

Dar es Salaam,

Tanzania

Simu: +255 - (022) 2123850/3/4/6

Faksi: +255 - (022) 2123180

Barua Pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: www.ewura.go.tz

KUTOKA KWA MHARIRI

Bw. Titus Kaguo

KARIBU katika toleo la pili la Jarida la Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ambalo lina habari nyingi za kuvutia.
Kwa wale ambao ni mara yao ya kwanza kuliona Jarida la EWURA, ninawahakikishia kuwa tumechagua njia hii miongoni mwa nyinginezo nyingi kuwafikia wananchi wengi kadri iwezekanavyo. Kwa njia hii, EWURA inakushirikisha na kukujuza kuhusu majukumu na kazi zake kuhusu sekta zinazodhibitiwa za umeme, mafuta, maji safi na taka, na gesi asilia.
Tunapenda, kadri tutakavyoweza, kujuza umma na kuuongezea uelewa kuhusu sekta zinazodhibitiwa. Wachache wenu wana uelewa mkubwa kuhusu haki na wajibu wa wateja na watoa huduma, pia Baraza la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (CCC). Baraza hilo lilianzishwa kisheria kutetea maslahi ya watumiaji wa huduma kwa sauti moja yenye nguvu kwa lengo la kuondoa kero zilizopo, tunakusihi uwasiliane na Baraza na kupata huduma.Kutokuwepo kwa mikataba ya hiari kati ya mteja na mtoa huduma, kunasababisha ongezeka la kero kwa wateja, na thamani ya malipo halali kwa ankara haijidhihirishi wazi. Kwa kuanzia, EWURA imeitaka TANESCO, na itaendelea kuhimiza watoa huduma wengine katika sekta zinazodhibitiwa kuwashirikisha watumiaji huduma katika hatua zote kuandaa mikataba ya hiari kati ya mteja na mtoa huduma.

Je, unajua kuwa endapo huridhiki na viwango vya huduma zinazotolewa na mtoa huduma katika sekta zinazodhibitiwa, unaweza kulalamika na kusikilizwa? Wengi wamefanya hivyo kupitia EWURA, wamesikilizwa na kupata suluhu ya kuridhisha. Pamoja na kusema hivyo, EWURA inahimiza watumiaji na watoa huduma kumaliza tofauti, malalamiko na migogoro miongoni mwao. EWURA imefungua tovuti www.ewura.go.tz ambapo taarifa nyingi na maelekezo yanapatikana. Huu ni ubao wetu wa matangazo. Unaweza kutufikia au kutupatia tafakuri kwa kutumia info@ewura.go.tz nasi tutakujibu mara moja. Aidha, EWURA imeanzisha Daftari la Wazi katika ofisi zake zilizoko katika jingo la Harbour View Towers, Mtaa wa Samora, Dar es Salaam. Tafadhali jikite katika tovuti yetu mara kwa mara au tutembelee ili ujuzwe. Habari ni silaha!

Katika robo mwaka ya tatu (Julai hadi Septemba, 2009), EWURA imeendesha semina nyingi kuhusu masuala ya udhibiti. Tumewafikia wabunge wote, watoa huduma za maji safi na taka wa mikoa yote Tanzania Bara, vyombo vya habari jijini Dar es Salaam, na wananchi wengi katika mikoa ya Ruvuma, Kigoma na Tabora. Lengo letu ni kuwafikia wananchi wa mikoa yote iliyobaki.
Jambo la kufurahisha, uelewa wa wananchi unaongezeka kila kukicha. EWURA haitakuwa kila pahala wakati wote, wewe ni mach na masikio yetu, tuambie au tuandikie ukiwa na shaka lolote au kama una taarifa itakayotuwezesha kufanya kazi yetu ya kukutumika vizuri zaidi.

Tunawapongeza wote wanaotupatia taarifa kuhusu ubora na bei za mafuta kufuatia bei elekezi zinazotolewa na EWURA mara kwa mara Ni dhahiri kuwa mmekuwa wazalendo na mmesaidia uchumi wetu na ustawi wa mali zetu hasa magari. Kupitia kwako, EWURA imekabiliana na vitendo vya uchafuzi wa mafuta kwa kiasi kikubwa. Kwa kuuunga mkono, EWURA inawachukulia hatua kali watoa huduma wasio waadilifu. Vitendo viovu vinaendelea kupungua.Ni matarajio yangu kuwa mtafurahia habari zilizomo katika toleo hili la Jarida mlipendalo.

KUTOKA DAWATI LA MKURUGENZI MKUU

Bw. Haruna Masebu

TOLEO hili linatoka wakati ambao kundi la kwanza la wafanyakazi wa EWURA ndio kwanza wamesherehekea miaka yao mitatu tangu wajiunge na EWURA, mnamo Septemba mosi 2009. Septemba 30 inakumbukwa kwani ndio ulikuwa ukomo wa msaada PPSDP kwa EWURA. Ukomo wa msaada huu wa PPSDP umekuja wakati ambapo EWURA imejijenga na kujizatiti na sasa inaweza kusimama na kujitegemea yenyewe. Tunazishukuru Serekali ya Tanzania na Benki ya Dunia kwa ufadhili. Wanayosababu ya kujivunia kuwa na Mamlaka ya udhibiti ya kiwango cha kimataifa kupitia ufadhili huu wa PPSDP. Matunda mengine ya PPSDP, (kama vile uundwaji wa mamlaka za udibiti za TCRA, SUMATRA, TCAA, FCC na FCC), yakijumuishwa katika mafanikio haya, kuna kila sababu ya kusema hongera Serekali ya Tanzani na Benki ya Dunia kwa kazi nzuri.

Toleo hili pia linakuja wakati ambapo Serekali imeniteua tena kuwa Mkrugenzi Mkuu wa EWURA kwa kipindi kinginena cha mwisho cha miaka mine. Natumia fursa hii kuwashukuru Wakrugenzi wa Bodi na wafanyakazi wote wa EWURA ambao kwa namna moja au nyingine walitengeneza mazingira yaliyopelekea Serekali kuona inafaa kuubakiza uongozi wa EWURA ulipo kupitia utezi wangu. Uteuzi huu imenigusa kipekee na umeonyesha imani kubwa aliyonayo Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, waziri mwenye dhamana juu ya EWURA. Hii ni kwa sababu Profesa Mwandosya ni mwanataalum mwenye uzoefu wa kutosha katika masula ya nishati na bila tashwishi yoyote ametoa mchango maridhawa katika kufanikisha mfumo wa udhibiti hapa nchini. Mathalani kuna wakati alikuwa na wajibu wa kuteua uongozi wa Mamlaka zilizokuwa chini ya Wizara ya Miundo Mbinu kama vile TCRA, TCAA, SUMATRA na sasa EWURA. Aksanteni Sana.

EWURA inaendelea kuleta mafanikio ikizingatia malengo yote ya kuundwa kwake. Mazingira ya udhibiti yameendelea kuwa ya uhakika na yanayotabirika, kwa kuzingatia nyenzo za udhibiti (kanuni na miongozo). Umakini wa EWURA katika kuzingatia mchakato wa udhibiti na ushirikishwaji wa wadau kumeipatia heshima na kukonga nyoyo za wanataaluma wa kimataifa katika Nyanja ya udhibiti. Washirika wengine wa udhibiti katika ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kusini (EAC, SADCC) na katika bara la Afrika kama vile AFUR, wameiona EWURA kama mshirika makini katika kutoa mchango wa kuzileta pamoja taratibu za udhibiti. Halikadhalika EWURA imekuwa ikiendelea kuongeza wigo wa shughuli zake kama vile kutoa elimu kwa umma, wabunge, viongozi mbalimbali na hata kwa waandishi wa habari na inafanya hivyo mara kwa mara.

Watoa huduma wengi sasa wanajua kuwa inapokuja kwenye suala la kuishawishi EWURA inapofanya maamuzi yake kitu muhimu ni hoja zenye nguvu na si vinginenvyo. Mara kadhaa maamuzi ya EWURA yametoa kinga madhubuti kwa watoa huduma na kwa Serekali dhidi ya lawama na shutuma kutoka kwa wananchi. EWURA mara nyingi imeshutumiwa na kulaumiwa pale inaporuhusu bei kupanda, na mara nyingi imezipokea shutuma hizo. Kwa mantiki hii EWURA imekuwa ikibeba mzogo wa lawama kwa niaba ya wadau wote.

Ufuatiliaji wa karibu wa mwenendo wa utoaji huduma umepelekea kuongezeka kwa ufanisi. Hakika EWURA iko mstari wa mbele katika kuleta mageuzi ya sekta zenye ukiritimba kama vile maji na umeme na hata zile zilizokuwa zinafanyakazi kwa mtindo wa “soko huria”, kuwa “soko la haki” kwa manufaa ya wote. Tafadhali endelea kusoma juu ya mageuzi haya katika kurasa zinazofuata.

KUELEKEA KWENYE UNUNUZI WA MAFUTA KWA PAMOJA

Na Titus Kaguo

SERIKALI ya Tanzania imedhamiria kuendelea na mpango wake wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja ili kulinda masilahi ya Taifa , licha ya upinzani kutoka kampuni za biashara ya mafuta (OMCs). Waziri wa Nishati na Madini, Mh. William Ngeleja, amesema maandalizi ya ununuzi huo yamefikia pazuri na mfumo huo unatarajiwa kuanza hivi karibuni.

Mh. Ngeleja anasema, madai yanayotolewa na OMCs kuwa Serikali haikufanya utafiti wa kutosha, hayana msingi, kwa sababu Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA), walifanya utafiti ili kujiridhisha na mfumo huo.

Mh. Ngeleja alitoa msimamo huo wa Serikali alipozungumza na wafanyakazi, menejimenti na wajumbe wa Bodi yaWakurugenzi wa TPDC Mwezi Agosti mwaka huu. ”TPDC imetushauri vizuri na tunashawishika kuwa ni hatua nzuri kwa maslahi ya Watanzania wengi na si kwa waagiza mafuta wachache,” alisema.

Alisema wanaopinga hatua hiyo ndio walikuwa mbele kukosoa na kuhoji safari za nje za wafanyakazi wa EWURA, walipokwenda huko kwa ajili ya kujifunza kinachofanywa na nchi zingine juu ya ununuzi wa aina hiyo na ndio hao sasa wanalalamika kuwa hakuna utafiti uliofanyika. Alisema kama mfumo huo utatekelezwa, hatua hiyo itaweza kupunguza gharama kwa kati ya asilimia 15 na 18, na kupunguza bei ya mafuta kwa mlaji na hatimaye mzigo kwa Watanzania.

Waziri pia alikanusha madai ya OMCs kuwa nchi haina miundombinu ya kutosha kusimamia ununuzi huo, kwa sababu iliyopo ni chakavu na haikidhi haja. “Ukweli ni kwamba, hata kwa miondombinu iliyopo ambayo wenzetu hawa wanasema haitoshi ni dhahiri haitumiki ipasavyo kwani ni asilimia 70 tu ya miundo mbinu iliyopo ndio inayotumika,” alisema.

Mh. Ngeleja alisema mwaka jana, meli 93 za mafuta ziliingiza mafuta katika bandari ya Dar es Salaam. Hata hivyo, utaratibu mpya ukianza, idadi ya meli zitakazoruhusiwa bandarini hapo itapungua hadi 55. Hii itapunguza msongamano na gharama za hifadhi bandarini.

Waziri alisema Serikali inaelewa, kwamba OMCs zinahofia kupoteza faida zilizokuwa zikipata kwa mfumo wa sasa wa ununuzi, ambao unaruhusu kila kampuni kuagiza kivyake.

Kwa mujibu wa Ripoti ya mwisho ya mshauri, utawekwa utaratibu mpya wa kusimamia utekelezaji wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja.

Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya (Mb) (Kulia) akijadiliana na Waziri wa Nishati na Madini, Mhesimiwa William Ngeleja (Mb), kabla ya kufunguliwa semina ya Wabunge mjini Dodoma Julai 12, 2009 huku Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Bw. Haruna Masebu (Kushoto) na Ofisa Mkuu wa Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Bw. Titus Kaguo wakisikiliza kwa makini.

Na Titus Kaguo

KATIKA juhudi za kumuunga mkono Rais Jakaya Mrisho Kikwete katika mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI kwa jumla, na kuzuia kuenea kwa maambukizi nchini, Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) imeanza kutoa elimu (mafunzo) juu ya kinga ya VVU/UKIMWI kwa wafanyakazi wake.

Uzinduzi wa mafunzo hayo ulifanywa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka, Bw. Haruna Masebu, na kuhudhuriwa na wafanyakazi wote. Katika tukio hilo, Bw. Masebu aliwahimiza wafanyakazi hao kujitolea kupima kwa hiyari na kupewa ushauri nasaha (VTC), kwa kutambua kuwa mtu kujua mapema afya yake ni jambo muhimu.

Bw. Masebu aliwahakikishia msaada wa kiafya wafanyakazi watakaobainika kuwa na virusi vya UKIMWI.

“Mamlaka itatoa msaada kupitia huduma nzuri ya afya kwa wafanyakazi wote watakaobainika kuathirika,” alisema Mkurugenzi Mkuu na kuongeza:” Pia tutahakikisha wanapata chakula bora na kuendelea na kazi zao kwa mujibu wa sheria.”

Bw. Masebu alisema mafunzo hayo ni kuitikia kaulimbiu ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwamba ‘Tanzania Bila UKIMWI Inawezwekana’. Ana matumaini kuwa kama elimu stahiki itatolewa kwa wafanyakazi wa EWURA, ni wazi watakuwa katika nafasi nzuri ya kuepukana na janga hili la kitaifa.

Kwa mujibu wa Bw. Masebu, Mamlaka itatoa mafunzo yanayotakiwa juu ya VVU/UKIMWI kwa watumishi wake kila miezi sita na kutokana na hilo, aliwataka wafanyakazi hao kuhakikisha kuwa wanahudhuria mafunzo hayo bila kukosa.

Mbali na watakaobainika kuambukizwa, Bw. Masebu, aliwataka watakaokuwa hawajaathirika, kujitolea damu kusaidia benki ya damu.

Tatizo la VVU/UKIMWI kwa mara ya kwanza liligundulika nchini mwaka 1983. Ugunduzi huo uliifanya Serikali ya Awamu ya Tatu chini ya Rais Mstaafu Benjamin Mkapa, kutangaza mwaka 1999 kuwa ugonjwa huu ni janga la kitaifa.

Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Bw. Haruna Masebu akichukuliwa damu kwa ajili ya kupima virusi vya UKIMWI kwa hiari wakati wa mafunzo ya kupambana na maambukizi ya UKIMWI kwa wafanyakazi wa EWURA.

DAWASA YAPEWA MUDA KUBORESHA HUDUMA ZAKE

Bi Violet Irama na Bw. Walter Geoffrey

MOJA ya majukumu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ni kufuatilia na kuhakikisha uboreshaji wa huduma zinazosimamiwa ikiwa ni pamoja na sekta ya maji.

Katika utekelezaji wa majukumu haya, Julai 10, 2009, EWURA kupitia Bodi yake ya Wakurugenzi iliiagiza Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya Dar es Salaam (DAWASA) kuboresha ugavi wake wa maji na huduma za majitaka kwa wateja katika maeneo inakohudumia, ikiwa ni pamoja na Jiji la Dar es Salaam na sehemu za Kibaha na Bagamoyo mkoani Pwani.

EWURA iliagiza kuwa kabla ya mwishoni mwa Juni 2010 Dawasa iwe imefanya mapitio ya viwango vyake vya sasa na njia inayotumika kiuendeshaji, kwa kuzingatia mabadiliko na mwenendo wa kichumi na kiufundi kama ilivyo katika Makubaliano ya mkataba kati ya DAWASA (mmiliki) na Kampuni ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASCO) ambaye ni mwendeshaji.

Masharti haya yaliwekwa ili kuhakikisha kuwa DAWASA inakuwa na viwango vya uhakika vya malipo ya maji na vinavyolipika na wateja ambavyo vitaiwezesha kulipia gharama za uendeshaji na matengenezo.

Pia, katika kuhakikisha kuwa huduma za DAWASCO zimepangwa vizuri na kutekelezwa kwa malengo ya kukidhi mahitaji ya wateja na DAWASA, EWURA kupitia agizo lake, imeielekeza DAWASA kupitia utendajikazi wake katika kufikia malengo katika mkataba wake na DAWASCO na kuiridhisha EWURA kabla Juni 30, 2010.

Ili kuhakikisha kwamba wateja wanatozwa kulingana na walichotumia, agizo linaitaka DAWASA kuongeza idadi ya wateja wenye mita kutoka 39,000 wa sasa hadi 104,000 kabla ya Januari 31, 2010 na masharti hayo yalisisitiza kwamba wateja wote wa Kimara, Kibaha, Katikati ya Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya Boko wawe na mita ifikapo mwishoni mwa Januari 2010.

Katika utekelezaji wa masharti hayo, DAWASA pia ilielekezwa kupitia na kuhakikisha inakuwa na Kanuni za Utendaji kama ilivyo katika mkataba baina yake na DAWASCO.

Ili kuhakikisha kuwapo kwa huduma nzuri kwa wateja wake katika maeneo yote ya utendaji na kuhakikisha kuwa hasara zinazotokana na kuvuja ovyo kwa maji na za kibiashara zinapunguzwa, agizo hilo linaitaka DAWASA kuwasilisha EWURA mpango wake wa kupunguza hasara kutoka asilimia 53 za sasa hadi chini ya asilimia 35 ifikapo Desemba 2013.

Masharti hayo yanasisitiza zaidi, kwamba DAWASA ihakikishe inapunguza kiwango cha maji yanayopotea bure kutoka asilmia 53 ya sasa hadi asilimia 40 ifikapo Juni 2010 kama inavyoonekana katika bajeti ya DAWASCO kwa mwaka 2009/10. Agizo linasisitiza kuwa haina budi ihakikishwe kuwa upotevu wa maji unabakia asilimia 40 kwa kiwango chochote cha malipo kitakachotumika baada ya Juni 30, 2010.

Katika kuhakikisha uhusiano mzuri kati ya wateja na mwendeshaji (DAWASCO) na upunguzaji wa malalamiko ya wateja, agizo hilo limejumuisha masharti yanayoitaka DAWASA kutoa uthibitisho kwa EWURA wa kuandaa na kutekeleza mpango wa kuwafikia wateja (elimu kwa mteja juu ya wajibu wao, mawasiliano, n.k.) kabla ya Desemba 31, 2009.

Katika utekelezaji wa masharti hayo, DAWASA inaelekezwa kuwasilisha EWURA taarifa ya utekelezaji wa mpango kila mwaka na itajumuishwa na mambo ya baadaye ya marekebisho ya bei ili yafikiriwe na EWURA katika kuifanyia tathmini.

Agizo hilo pia linaitaka DAWASA kuendelea kuipa EWURA taarifa juu ya hali yake ya kifedha na uendeshaji kwa mujibu wa mahitaji ya Ewura. Taarifa hii itatumika na Ewura kutathmini utendaji wa DAWASA kwa kulinganisha na watumiaji wengine na kuboresha utendaji wake.

Pia, tathmini itafikiriwa na EWURA katika kutathmini utekelezaji au vinginevyo maombi ya baadaye katika marekebisho ya bei.

Agizo hilo la EWURA lilitolewa kwa DAWASA baada ya maombi ya DAWASA ya kuongeza bei ya matumizi ya maji na kuidhinishwa kutoka shilingi 654 kwa meta ya ujazo hadi shilingi 850 kwa maji ya kunywa na ongezeko la shilingi 227 kwa meta ya ujazo kwa majitaka. Viwango vipya vilianza Agosti mosi, 2009.

WAZIRI wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya amemteua Bw. Haruna Masebu kuongoza Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kwa mara ya pili kuongoza kwa miaka minne kuanzia Januari mosi 2010.

Uteuzi huo utamwezesha Bw. Masebu kuimarisha mambo aliyoanzisha, kuhakikisha kuwa nchi yetu inakuwa na mfumo bora wa kudhibiti mafuta ya petroli, umeme, gesi asilia na majisafi na majitaka ambao utakuwa wa wazi, haki, wenye matokeo mazuri na ufanisi mkubwa.

Bw. Haruna Masebu aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA na mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa EWURA kwa mara ya kwanza Januari 2006.

WAZIRI wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya amemteua Dkt. Geoffrey Mariki kuwa Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kuanzia Agosti Mosi 2009.

Dkt. Mariki mwenye uzoefu wa miaka 35 kama Mhandisi wa Umeme hususan kwenye ufuaji, usambazaji na ugavi, kwa miaka 23 amefanya kazi katika sekta ya viwanda vya kimataifa katika nyanja mbalimbali za masuala ya nishati na ugavi wa maji na matumizi ya viwanda kwa maendeleo. Pia ana uzoefu katika kupanga, kutekeleza, kuongoza, kusimamia na kutathimini miradi.

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imemwajiri Meneja mpya wa Fedha na Utawala (FAM), Bi. Margareth Naiunguishu Soikan Mollel, ambaye anauzoefu mkubwa katika taaluma ya kifedha. Bi. Mollel ambaye ana Shahada ya Uzamili ya Utawala wa Biashara katika Fedha kutoka Chuo Kikuu cha Charles Sturt University cha Australia aliyoipata mwaka 2006 anatarajiwa kuboresha masuala ya fedha na utawala ndani ya Mamlaka.

Bi. Mollel ni mmoja ya Maofisa wazuri waliowahi kuajiriwa ndani ya Idara Fedha ambaye ataongeza ubora katika mifumo ya kifedha iliyopo. Bi. Mollel atawajibika kwenye utendaji wa masuala ya fedha, malengo ya mipango ya mamlaka yakiwemo kuwasimamia watumishi waliopo katika idara ya Fedha na Utawala na kuangalia utayarishaji wa ripoti za Fedha na utunzaji wake. Pia anatarajiwa kufanya kazi kwa ujirani na idara zote za mamlaka kwa kutoa taarifa mapema zinazowezesha mamlaka kufikia uamuzi mwafaka.

EWURA YAENDESHA MAFUNZO KWA MAMLAKA ZA MAJI

Bw. Karim Ally na Mhandisi Nyirabu Musira

KITENGO cha Maji cha Mamlaka ya Udhibiti Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kimeanza kutoa mafunzo ya usimamizi wa matumizi ya maji nchini Tanzania. Awamu mbili za mafunzo hayo zilifanyika Mwanza na Morogoro kati ya Juni na Julai 2009, na awamu ya tatu inapangwa kufanyika Mbeya kabla ya mwisho wa Septemba 2009.

Mafunzo hayo yanafadhiliwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP). Malengo ya mafunzo hayo ni kusambaza taarifa juu ya wajibu na kazi za EWURA kwa maofisa wasimamizi wa matumizi ya maji, pia kuwafahamisha kanuni mbalimbali za udhibiti.

Mafunzo ya Mwanza ambayo yalifanyika katika hoteli ya La Kairo kuanzia Juni 8 hadi 12, 2009, yalikutanisha wafanyakazi na maofisa kutoka mikoa na wilaya za mikoa ya Kagera, Kigoma, Mwanza, Mara, Tabora na Shinyanga.

Mafunzo ya Morogoro yalifanyika katika hoteli ya B-Z kuanzia Julai 20 hadi 24, 2009 na kukutanisha washiriki kutoka Morogoro, Lindi, Mtwara, Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga na Kampuni ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASCO) kutoka Dar es Salaam.

Kila kitengo cha huduma ya maji kiliwakilishwa na takriban watu watatu wafanyakazi wa ngazi ya menejimenti na ofisa mmoja anayeshughulikia uandaaji ripoti za kuwasilishwa EWURA au wizarani.

Mada mbalimbali ziliwasilishwa na wafanyakazi wa EWURA wakiwamo baadhi ya Wakurugenzi wa Kanda, mameneja na watumishi wengine waandamizi. Mada zilizowasilishwa zilikuwa na nia ya kuwapa washiriki maarifa juu ya usimamizi lakini pia kuwafahamisha wajibu wao wa usimamizi kama watoa huduma.

Mada zilizowasilishwa ni pamoja na Wajibu na Majukumu ya EWURA; Taratibu na Mahitaji ya Maombi ya Leseni, Makubaliano ya Utendaji baina ya EWURA na Watumiaji Maji, Miongozo ya Matumizi ya Viwango vya Bei na Mchakato wa Tathmini, Uandaaji Ripoti na Muda wa Kuwasilisha Ripoti, Miongozo ya Kuandika Mpangokazi wa Biashara na matumizi ya Kompyuta kama zana kuu ya Uongozi.

Washiriki wa mafunzo hayo walijadili na kuibua masuala mengi juu ya mada zilizowasilishwa ambayo yalipata ufafanuzi na majibu kutoka kwa wafanyakazi wa EWURA na mwakilishi wa Wizara.

Mwisho wa mafunzo, washiriki walieleza kuridhishwa kwani baada ya kuelewa umuhimu wa matumizi ya nyaraka mbalimbali zinazotakiwa na EWURA na Wizara na kufikia maazimio ya kuhakikisha unakuwapo utaratibu wa kuwasilisha ripoti na nyaraka kwa wakati unaotakiwa na EWURA na Wizara.

Pia watumiaji ambao hawajaomba leseni, walitakiwa kujaza na kuwasilisha fomu EWURA ifikapo mwishoni mwa Septemba 2009. Washiriki pia walitakiwa kutathmini mafunzo hayo kwa kujaza dodoso walizopewa, ambapo wengi wao walikuwa na mawazo ya jumla kuwa mafunzo hayo yalikuwa mazuri na muhimu kwa matumizi ya maji.

Baadhi yao walikwenda mbali na kupendekeza kuwa Ewura iendeshe mafunzo kama hayo angalau mara moja kwa mwaka.

KUBADILISHANA UZOEFU NA KUANZISHA USHIRIKIANO KUHUSU MBINU BORA ZA UDHIBITI NI LAZIMA

Na Sirili Massay

MHESHIMIWA Profesa Mark Mwandosya (Mb), Waziri wa Maji na Umwagiliaji, ambaye pia ni Waziri mwenye dhamana na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), aliongoza ujumbe kwenda Guyana, Jamaica na Brazil.

Madhumuni ya ujumbe huo katika nchi za Latini Amerika ilikuwa ni kubadilishana na kupata uzoefu kuhusu mbinu bora za udhibiti na masuala ya ushindani kutoka nchi ambazo zimekuwa ni mfano wa kuigwa katika mambo ya ubinafsishaji na udhibiti katika miaka ya kati ya 1980. Kulikuwa na mambo mengi muhimu ya kujifunza kutoka nchi ndogo kama Jamaica na Guyana, na pia kutoka nchi kubwa kama Brazil. Vivyo hivyo, mtu mwingine anaweza kujifunza mambo mengine muhimu kutoka nchi ambazo ubinafsishaji umeshindwa kuonyesha faida, na pia kutoka nchi ambazo udhibiti wa soko huria umefanikiwa.

Ujumbe wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) katika ziara hiyo ulijumuisha: Balozi wa Tanzania nchini Brazil, Dk. Joram Biswaro, Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Bw. Haruna Masebu, Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA, Bi. Lucy H. Sondo, pamoja na maofisa wengine wa ngazi za juu kutoka EWURA na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Prof. Mwandosya amekuwa mstari wa mbele katika kuleta mabadiliko katika sekta za nishati na maji. Ni mmojawapo wa wabunifu wa mifumo ya udhibiti nchini Tanzania. Amekuwa Waziri mwenye dhamana ya SUMATRA, TCRA, TCAA na EWURA.

Nchini Guyana, awamu ya kwanza ya ubinafsishaji wa huduma za maji na nishati ulishindwa kuleta ufanisi. Wizara husika ziliendelea kutoa leseni na kupitisha tozo na mamlaka ya udhibiti haikuwa imepewa nguvu za kutosha. Hali hiyo inajionyesha pia visiwani Jamaica ambapo mamlaka ya udhibiti haikuwa na utaratibu dhabiti wa utekelezaji wa majukumu yake. Nchini Brazil, Serikali, mamlaka za udhibiti na pia watoa huduma wanashirikiana kwa karibu sana, na wanaheshimu na kutambua majukumu ya kila mmoja yalivyowekwa kisheria. Wamekubaliana kuruhusu mifumo iliyowekwa ifanye kazi, kama ikishindwa kuleta tija na ufanisi, wanakaa kwa pamoja na kuiboresha. Hakuna hata mmoja anayejaribu kuharibu kazi ya mwingine. Mambo mengi muhimu ya kujifunza yamepatikana kutoka nchi hizi tulizotembelea na mapendekezo ya ujumbe wa Tanzania yatasaidia sana katika kushawishi na kuboresha mifumo yetu iliyopo pale panapowezekana.

Nchini Guyana, na kutambua utaalamu wake, Prof. Mwandosya alikaribishwa kuhudhuria mkutano wa Kamati Teule ya Guyana ya Mkakati wa kulinda Mazingira na Kuzuia Mabadiliko ya Hali ya Hewa ambao ulifanyika wakati akiwa anatembelea Guyana. Alipewa nafasi ya kukutana na Mheshimiwa Bharrat Jagdeo, Rais wa Guyana, Mheshimiwa Samuel Hinds (Mb), Waziri Mkuu wa Guyana, na Mheshimiwa Irfaan Ali (Mb), Waziri wa Makazi na Maji. Ujumbe ulitembelea baadhi ya mamlaka za udhibiti, watoa huduma, pamoja na Chuo Kikuu cha Petrobras nchini Brazil. Ujumbe ulifanikisha mawasiliano kwa ajili ya uendelezaji endelevu wa rasilimali watu na vyombo mbalimbali, ufuatiliaji wa hayo unafanywa na Ubalozi wa Tanzania nchini Brazil.

Umuhimu wa kuwapatia mafunzo wadhibiti ili kuongeza uwezo wao na kuwafanya waweze kutoa maamuzi stahiki upo wazi, hasa kwa wadhibiti wapya katika chombo kama EWURA. Kuna mambo mengi katika sekta mbalimbali yanayomkabili mdhibiti. Udhibiti ni swala jipya na ambalo bado halijaeleweka vizuri, na litakuwa na changamoto nyingi kutoka sehemu mbalimbali hata kama faida zake zinaonekana wazi. Hivyo basi ni muhimu kwa mdhibiti kufanya mambo sahihi kuanzia mwanzo, na kuyafanya vizuri ili mafanikio yake yaweze kuonekana. Mabadiliko huwa yanachukua muda ili yaweze kuonekana.
Baadhi ya changamoto zinazozikumba mamlaka za udhibiti kwenye nchi nyingi ni kutoka kwenye makampuni yenye ukiritimba wa soko. Makampuni haya yanaweza kuwa ya Serikali au ya binafsi. Makampuni binafsi, hasa yale yaliyofanya biashara kabla mamlaka za udhibiti hazijaingia kwenye soko, huwa na uzito kukubaliana na mabadiliko, hasa mabadiliko yenye lengo la kumlinda mteja ili apate bidhaa na huduma zenye ubora. Pia kampuni nyingi hazipendi kutoa taarifa ili kulinda biashara zao. Vile vile wapo baadhi ya watunga sera wa serikalini ambao hawapendi kuona mamlaka ya udhibiti ikifanya

kazi zake barabara, hasa pale ambapo Sheria haiko wazi katika kuainisha wazi majukumu ya mamlaka ya udhibiti. Hii inatokana na hisia kwamba mamlaka za udhibiti zinapokonya kazi zilizokuwa zinafanywa na Wizara na hivyo Wizara zitadhoofika.

Duniani kote, njia bora ambayo imekubalika ya kujifunza haraka ni kupitia kubadilishana uzoefu kati ya nchi na nchi. Kama usemi usemavyo, "Hauhitaji kugundua gurudumu … wakati magurudumu tayari yanakimbia!". Uzoefu wa kiutendaji na changamoto kutoka nchi mbalimbali zitasaidia katika kutafuta njia bora za kiutendaji na kuhimili changamoto za nchi nyingine kulingana na mazingira ya nchi husika. Hali hii, itahusisha ujengwaji wa ushirikiano na taasisi mbalimbali za kitaifa na zile za nchi jirani ili kuboresha mitaala yao ya sasa.
EWURA imefanikiwa kuweka mtandao wa kubadilishana taarifa na misaada ya kitaalamu na taasisi zingine za udhibiti wa nishati na maji kutoka nchi mbalimbali. Lengo ni kuboresha sera, sheria na udhibiti wa sekta za nishati na maji. Pia makampuni binafsi kutoka nchi kama Brazil, mfano Electrobras, yameonesha njia ya kutaka kuja kuwekeza Tanzania. Katika kuhitimisha ziara yetu ya katika nchi za Caribbean na Latini Amerika, Prof. Mwandosya alisema "Ni lazima kubadilishana uzoefu na kuanzisha ushirikiano kuhusu mbinu bora za udhibiti".

EWURA inadhibiti sekta muhimu sana kwa uchumi wa Tanzania. Sekta hizo ni maji safi na maji taka, umeme, mafuta ya petroli na gesi asilia. Maji in muhimu sana kwa maisha ya viumbe. Umeme ni muhimu kuwaangazia watu na shughuli mbalimbali za kimaendeleo. Mafuta ya petroli ni muhimu kwa sekta ya usafirishaji na kuendeshea mitambo mbalimbali. Gesi asilia inasaidia sana katika uzalishaji wa umeme na kuwa chanzo cha nishati kwa baadhi ya viwanda kama kiwanda cha saruji n.k. Sekta hizi ni muhimu sana na udhibiti wake unatakiwa kufanywa na watu wenye uwezo na waliopatiwa mafunzo ya kutosha, vinginevyo uchumi wa nchi unaweza kuwa katika hatari kutokana na udhibiti usio makini.

Rais Bharrat Jagdeo wa Guyana (kushoto) akijadiliana na Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya mjini Georgetown-Guayana Septemba 2009.

CHANGAMOTO KATIKA UTOAJI LESENI ZA BIASHARA YA MAFUTA

Na Amina Shamte

MAMLAKA ya Usimamizi wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imelenga kuwa ifikapo mwaka 2010, wafanyabiashara ya mafuta wawe wamepewa leseni. Kwa kiasi kikubwa zoezi la utoaji leseni limepokewa vizuri. Mathalan, hadi katikati ya Agosti 2009, Mamlaka imeweza kushughulikia na kutoa leseni 430 kati ya maombi 1,101 ya waombaji wa uuzaji wa rejareja na wa jumla walioomba kati ya Novemba 2006 na Agosti 2009. Miongoni mwa hawa, 386 (kati ya 983) ni waombaji wa leseni za biashara ya reja reja na 44 kati ya 118 ni wa jumla.

Kwa upande mwingine, zoezi la utoaji leseni linakabiliwa na changamoto kubwa. Hadi kufikia Septemba 2009, idadi kubwa ya waombaji wa rejareja wameshindwa kutekeleza moja ya mahitaji makuu muhimu, kama vile kuwasilisha uthibitisho wa umiliki na matumizi ya ardhi kwa ajili ya biashara ya rejareja.

Kwa bahati mbaya, vibali vingi vya umiliki wa ardhi vilivyowasilishwa na waombaji havithibitishi uendelevu wa vituo vya mafuta na hakuna hata idhini ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi iliyowasilishwa. Hivyo maombi kama hayo hayawezi kufikiriwa kwa ajili ya kutolea leseni. Baadhi ya waombaji wanawasilisha nakala za vibali vyao ambavyo havina uthibitisho wowote na hivyo kusababisha ugumu kwa Mamlaka kuamua uhalali wao.

Waombaji wengine waliwasilisha nakala halali zilizothibitishwa, lakini zenye matumizi mengi au ambazo hazioneshi umiliki wa shughuli moja katika ardhi husika. Mathalan, ambako Sheria za Mipango Miji au Nchi kama zilivyofanyiwa mabadiliko mwaka 1993 zinaonesha kuwa Kundi F la Matumizi, Daraja (a) ni kwa ajili ya Vituo vya Mafuta, baadhi ya waombaji wanawasilisha vibali ambavyo ni vya matumizi ya Kundi P-kinyume cha sheria.

Pia, waombaji wengi wa leseni za jumla, walishindwa kuwasilisha vigezo vya msingi vya kuomba leseni, vinavyohitaji kuwasilishwa kwa uthibitisho wa uwezo wa kifedha na umiliki wa eneo la mafuta, au mpangilio muafaka wa huduma na waendeshaji katika eneo husika.Licha ya changamoto hizo hapo juu, Mamlaka imechukua hatua kadhaa za kuhakikisha kuwa waombaji wanawasilisha EWURA nyaraka zote zinazotakiwa, kabla ya muda kwisha. Moja ya hatua hizo ni kupitia upya utoaji leseni kwa ajili ya leseni za rejareja, kwa lengo la kuruhusu utoaji leseni kwa masharti.

Nyingine ni ya kuwafahamisha waombaji juu ya mahitaji ya msingi na masharti ambayo yanatakiwa kutimizwa kwa kipindi maalumu kilichowekwa-kupeleka kumbukumbu kupitia barua, matangazo magazetini na vipindi vya redio.

Baadhi ya waombaji ambao waliwasilisha vibali vyao ambavyo havithibitishi uendelevu wa vituo vya mafuta wameshauriwa na EWURA kuomba mabadiliko ya matumizi ya ardhi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Hata hivyo, haina budi kufahamika kuwa mchakato wa mabadiliko ya matumizi ya ardhi, ni mrefu na uthibitisho wa mwisho wa mabadiliko ya matumizi ya ardhi yanatolewa na waziri mwenye dhamana.

Haina budi pia kusisitizwa, kuwa ili kufikia malengo yake kwa utoaji leseni kwa wafanyabiashara wote wa mafuta ifikapo mwaka 2010, Mamkala imechukua pia jukumu la kuwasilisha orodha ya waombaji wote katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ili ama kuthibitisha au la, kuwa waombaji hao wana uthibitisho wa kujenga vituo vya mafuta katika viwanja husika.

Kwa kiasi kikubwa, shughuli ya utoaji leseni kwa biashara hiyo ya mafuta imekuwa na changamoto. Lakini bado ipo haja ya kushukuru ukweli kuwa kabla ya EWURA, ni wauzaji wa jumla tu wa mafuta ndio waliokuwa wakipata leseni. Leo, asilimia 39 ya wauzaji wa rejareja nchini wana leseni na zoezi hilo ni endelevu.

Pia, vituo vya mafuta hivi sasa vinaendeshwa kwa viwango vilivyowekwa na EWURA, na ambavyo vinakaguliwa mara kwa mara.

MATUKIO KATIKA PICHA

1

2

3

4

5

1. Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Bw. Haruna Masebu akitoa hotuba baada ya Waziri wa Nishati na Madini, Mh. Williiam Ngeleja (Mb) kufungua semina kwa wabunge juu ya shughuli za EWURA.

2. Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Bw. Arthur Mwakapugi (kushoto) akibadilishana mawazo na Mjumbe wa Bodii ya EWURA, Bi. Lucy Sondo (Kulia) kabla ya kufunguliwa kwa semina juu ya shughuli za EWURA iliyofanyika mjini Dodoma Jullai 12, 2009. Wa pili kutoka kushoto ni Kamishna wa Nishati na Petroli, Bw. Bashiri Mrindoko na Mkurugenzi wa Petroli wa EWURA, Bw. Sirili Massay.

3. Mkurugenzi wa Fedha na Rasilimalli Watu wa EWURA, Bw. Paskali Massawe akicheka huku Mkurugenzi wa Petroli Bw. Sirili Massay pengine alikuwa anamweleza kwa utani kwamba: “Nitaweza kuwashawishi Wabunge katika mada yangu? Kushoto ni Kamishna wa Nishati na Petroli , Bw. Bashiri Mrindoko.

4. Wahariri wakisikiliza maelezo ya awali kutoka kwa Mkuu wa Idara ya Mawasiliano na Uhusiano ya EWURA, Bw. Titus Kaguo kabla ya mkutano wa wahariri huo kufunguliwa na Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Bw. Haruna Masebu (hayupo pichani) Septemba 2009..

5. Mbunge wa Jimbo la Sumve, Bw. Richard Ndassa (CCM), akichangia jambo katika semina ya wabunge.

6. Mhariri Mkuu wa Gazeti la HabariLeo Bw. Joseph Kulangwa, akimuuliza swali Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Bw. Haruna Masebu katika mkutano wa wahariri. Wengine ni Bw. Denis Msacky ambaye ni Naibu Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Mwananchi, Bw. Theophil Makunga, Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Mwananchi na Bw. Gabby Mgaya ambaye ni Mhariri Msaidizi wa Gazeti la Daily News.

7. Wajumbe wa Bodi ya EWURA , Baraza la Ushauri la EWURA (CCC), Baraza la Serikali (GCC) na maofisa wa EWURA wakisikiliza mada juu ya shughuli za EWURA

8. Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Bw. Haruna Masebu, akifafanua jambo wakati alipokutana na wahariri wakuu wa vyombo vya habari Dar es Salaam mwezi Septemba 2009 ili kubadilishana mawazo juu ya utendaji kazi wa EWURA, Kulia ni Meneja wa Fedha na Utawala wa EWURA, Bi. Naiungishu Mollel na kutoka kushoto ni Mkaguzi wa EWURA wa Ndani wa Mahesabu Bw. Fred Msemwa na Mkurugenzi wa Petroli, Bw. Siril Massay.

9. Mkurugenzi Mdhibiti Uchumi wa EWURA, Bw. Felix Ngamlagosi (kulia) akijadiliana na Meneja wa Uchmbuzi wa Mahesabu na Uchumi , Bw. James Andilile (katikati) na Mkurugenzi wa Huduma za Maji na Majitaka, Bw. Mutaekulwa Mutegeki jinisi ya kukliweka bango la EWURA katika ukumbi wa Pius Msekwa.

EWURA YAPIGA HATUA KATIKA KUMLINDA MLAJI

Na Michael Mshighwa

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepiga hatua kubwa katika kumlinda mlaji. Hadi Juni 30, 2009, EWURA ilishapokea jumla ya malalamiko 120, kati yao, 53 yalitoka kwa wateja wa maji – na 27 yalishughulikiwa vizuri.

Sekta ya nishati ilipokea malalamiko 34, ambapo 12 yalitatuliwa. Sekta ndogo ya biashara ya mafuta ilipokea jumla ya malalamiko 34 ambapo 23 yalitatuliwa. Jedwali namba moja chini hapa linaonesha asilimia ya malalamiko yaliyopokewa na kutatuliwa katika kipindi kilichomalizika Juni 30, 2009.

Jedwali 1: Malalamiko yaliyopokewa na kushughulikiwa

Jedwali 1 hapo juu linaonesha asilimia ya malalamiko



JEDWALI 1 - Malalamiko yaliyopokelewa vs yaliyoshugulikiwa

yaliyotatuliwa dhidi ya yaliyopokewa katika kipindi kilichomalizika Juni 30, 2009.

Malalamiko kutoka kwa walaji wa sekta zinazodhibitiwa na EWURA yanatofautiana kwa ugumu katika masuala yanayolalamikiwa.

Baadhi ya malalamiko yanatatuliwa kirahisi na haraka. Mengine hata hivyo, yanaweza kuwa magumu zaidi, yakahitaji msaada kutoka kwa watu mbalimbali na matokeo yake yatatumia muda mrefu zaidi na magumu kuyatatua.

Kitengo cha malalamiko cha EWURA, hivi sasa kinapokea malalamiko hayo kupitia barua, faksi, simu, intaneti au walalamikaji kufika wenyewe. EWURA inashughulikia malalamiko hayo kwa ndani ikitumia utaratibu wa kuanzia chini kwenda juu kutoka



JEDWALI 2 - Aina ya malalamiko yaliyo pokelewa hadi 30 Juni 2009

Kitengo cha Huduma kwa Wateja hadi uongozi wa juu wa Mamlaka na kufuatiwa na uamuzi wa Bodi ya Wakurugenzi.

Agizo la Bodi kuhusu malalamiko hayo lina nguvu kama ambazo zinatumiwa na Mahakama Kuu ya Tanzania. Malamiko yanayopokewa ni kama yanavyooneshwa katika jedwali 2.

Jedwali 2: Aina ya malalamiko yaliyopokewa hadi Juni 30, 2009

Katika hatua za awali, utatuzi wa malalamiko unahusisha barua, faksi, barua pepe au simu. Barua ndizo zinatumika zaidi. Kwa mara nyingi barua na nakala ya malalamiko hupelekwa kwa mtoa huduma kutaka maelezo ya ilipofikia kushughulikiwa.

Mawasiliano ya simu mara nyingi yamekuwa yakitumika kujadili malalamiko, kuuliza maswali, au kutoa maombi maalumu. Majibu kutoka kwa mtoa huduma ndio hutoa mwanga wa hatua zaidi za kuchukuliwa kama kuna ulazima. Matokeo yake yanaweza kuhusisha upunguzaji wa bili, uombaji

radhi au ufafanuzi au kazi kufanyika bure kwa lengo la kurekebisha kosa.

Kama kitengo kitashindwa kufanya hivyo, suala hilo litapelekwa kwa uongozi wa juu wa Mamlaka ili kusikilizwa. Wakati wa kusikilizwa malalamiko, mchakato unakuwa ni wa pande mbili kuelewana kirafiki. Katika hilo kama hakutakuwa na maelewano ya kirafiki, pande hizo mbili zitatakiwa kufika mbele ya uongozi wa juu wa Mamlaka au ofisa mkuu au mwakilishi aliyeidhinishwa.

Uongozi wa menejimenti utawasilisha matokeo yake kwa Bodi ya EWURA kwa hatua. Bodi nayo itatoa uamuzi wa malalamiko ambao utatekelezwa na uongozi wa Mamlaka. Pale ambapo upande mmoja hautaridhika na uamuzi wa Bodi una haki ya kukata rufaa katika Baraza la Ushindani (FCT).

EWURA hivi sasa inakabiliwa na changamoto nyingi kuhusu utatuzi wa malalamiko. Ukosefu wa hifadhi nzuri ya ushahidi kwa upande wa mlalamikaji kuonesha kuwa zimekuwapo juhudi za kutatua matatizo na mtoa huduma kama inavyotakiwa na sheria ni moja ya matatizo sugu.

Matokeo yake, EWURA katika hali yoyote, iko radhi kupeleka suala hilo kwa mtoa huduma kwa ajili ya kufikiriwa, kuamuliwa na/au kutolewa ufafanuzi. Changamoto nyingine ni majibu na ushirikiano dhaifu kutoka kwa watumiaji. Katika matukio mengi, watumiaji ama huchelewa kujibu au hawajibu kabisa, hata kama wakipelekewa barua za kuwakumbusha.

EWURA haitaruhusu watumiaji kutumia vibaya mchakato wa kisheria na mara zote itaendelea kuzingatia majukumu yake ya dhati ya kuhakikisha taaluma ya hali ya juu inatumika na huduma zinatolewa kwa wakati ikiwa ni pamoja na kutatua migogoro kwa wakati muafaka. Kwa kufanya hivyo, Mamlaka, pamoja na mambo mengine, inazingatia kanuni muhimu ya utawala wa sheria, ambayo inasema, kucheleweshaa haki ni kunyima haki.

Watoa huduma na walaji wakihudhuria mkutano wa taftishi juu ya masuala ya mafuta.

HONGERA, WABUNGE WAIPONGEZA EWURA

Na James Andilile

ILIKUWA Julai 12, 2009 EWURA ilipopata fursa nzuri ya kukutana na wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mjini Dodoma. Wabunge hao walipongeza juhudi zinazofanywa na Mamlaka hii katika kutoa huduma na kutekeleza wajibu wake kama msimamizi wa nishati na maji ya Taifa hili.

Pongezi hizi zilitolewa katika semina ya siku moja mjini Dodoma. Ambapo Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Bw. Haruna Masebu, alielezea jinsi EWURA inavyotekeleza Sheria namba 414 ya Tanzania .

Akizungumzia mabadiliko ya usimamizi nchini Tanzania, Bw. Masebu alisema usimamizi wa uchumi nchini Tanzania ulihamasishwa na uamuzi wa Serikali kuingia katika uchumi wa soko huria.

“Mabadiliko ya mwelekeo wa jinsi uchumi unavyotaka kusimamiwa na kuendeshwa, yalisababisha kuwapo kwa tafsiri nyingine ya dhima ya Serikali,” alisema na kuongeza kuwa matokeo ya jukumu la Serikali kutafsiriwa upya ni kwamba sasa itawajibika katika kuunda sera na kuiacha sekta binafsi iongoze ujenzi wa uchumi wa nchi.

Katikati ya soko huria, mwaka 1999 serikali ilichukua uamuzi wa makusudi wa kuendeleza na kuanzisha Sera ya Ushindani ambayo, miongoni mwa mambo, ikawa inalenga kuanzisha kanuni za kulinda mazingira ya soko huria,” alisema.

Pia akasema Sera ya Ushindani imeweza kugundua umuhimu wa kuwa na ushindani wa haki katika kuleta ufanisi sokoni. Akirejea sera hiyo, alisema imeonesha palipo na ushindani wa kutosha katika uzalishaji na utoaji huduma, soko huachwa lijiendeshe lenyewe.

Hata hivyo, alisema kwa kujiamini kuwa, sera hiyo hiyo imethibitisha kuwa kuliko na ushindani hafifu, vyombo vya usimamizi havina budi kuanzishwa. Hicho ndicho kilichosababisha kuzaliwa kwa EWURA, TCRA, TCAA, SUMATRA, FCC na FCT.

“Kuanzishwa kwa vyombo hivi kulilenga kulinda maslahi ya mihimili mitatu katika usimamizi wa walaji wake na wawekezaji,” aliongeza. Bw. Masebu aliwaambia washiriki, kuwa usimamizi ni mbadala wa ushindani wa soko. Usimamizi unahakikisha kuwa soko huria linafanya kazi vizuri kwa maslahi ya wengi. “Ni kupitia usimamizi ndipo maslahi ya kila mdau yatakapohakikishwa,” alisema.

Bw. Masebu alisisitiza kuwa “katika Dunia ya leo, watu hawazungumzii tena soko huria bali soko la haki.”

Bw. Felix Ngamlagosi, Mkurugenzi wa Mdhibiti Uchumi wa EWURA naye alisema, “katika Dunia ya leo, usimamizi ni muhimu, bila kujali kama huduma inatolewa na sekta binafsi au ya umma, kwani usimamizi unalenga katika ufanisi.”

Ngamlagosi alieleza zaidi kuwa katika kutekeleza Sheria ya EWURA namba 414, Mamlaka inakabiliwa na changamoto nyingi, zikiwamo za ukosefu wa viwango muafaka vya bei, upungufu wa huduma za kutosha kwa Watanzania wengi, ukosefu wa usimamizi wa kisekta na haja ya Ewura kuheshimu makubaliano yote yaliyosainiwa kabla haijaanzishwa.

Akizungumza katika semina hiyo, Bw. Massay – ambaye ni Mkurugenzi wa Petroli wa EWURA – alisema Serikali imechukua uamuzi wa uagizaji wa pamoja wa bidhaa za mafuta nchini. “Kwa sasa, EWURA ikishirikiana na wadau wengine inaangalia njia bora zaidi ya kutekeleza hilo,” alisema. Pia Bw. Massay alieleza kuwa Ewura inapanga kununua na kuanzisha maabara zinazotembea za kupima mafuta, ili kudhibiti uchakachuaji mafuta unaofanywa nchini.

“EWURA inafanya kazi nzuri,” alisema Mhe. Daniel Nsanzugwanko. Hata hivyo, alitahadharisha kuwa utekelezaji wa ununuzi huo wa mafuta kwa pamoja ukifanywa na mtu yeyote utasababisha mshtuko sokoni na kukatisha tamaa wawekezaji. Vivyo hivyo Mhe. Mhonga akizungumzia sekta hiyo, alisema adhabu zinazotolewa kwa wafanyabiashara wanaokutwa wakifanya vitendo viovu katika biashara hiyo ni nyepesi na haziwezi kukomesha tabia hiyo.

"Vituo vya mafuta vinavyopatikana vikiuza mafuta yaliyochakachuliwa havina budi kufungwa milele na kubandikwa mabango yanayosema sababu za kufungwa huko, ili kuufumbua macho umma kuhusu uhalifu huu," alisema.

Pia Mhe. Ndassa aliitaka Ewura kufungua ofisi za kanda nchini kote ili huduma zao ziwafikie wananchi wengi. "EWURA na Serikali hawana budi kuharakisha utaratibu wa ununuzi mafuta kwa pamoja kwa ajili ya maslahi ya uchumi wetu," alisisitiza.

Kwa upande wake, Mhe. Zambi – akizungumzia viwango vya bei ya umeme – alisisitiza kuwa "EWURA haina budi kuangalia njia za kuhakikisha umeme unakuwa nafuu kwa Watanzania masikini na kuongeza juhudi za kujulikana kwa umma kwa sababu haijulikani kwa wengi."

Akizungumzia kazi za EWURA, Mhe Zitto aliitaka Serikali kutizama muundo wa Sheria ya mpya ya gesi ambao utakuwa na maslahi ya Taifa. "Maslahi ya Taifa hayana budi kupewa kipaumbele kwa kupitisha sheria kama hiyo," alionya Mh.Zitto.

Kwa upande wake Mh. Malomba alikuwa anamaoni kuwa kutokana na shughuli nyingi za EWURA kuihusisha Wizara ya Nishati na Madini, ni vyema EWURA ikawa inawajibika kwa Wizara hiyo tofauti na ilivyo hivi sasa. EWURA kwa sasa inawajibika kwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Hata hivyo, akitoa ufafanuzi kuhusu muundo huo, Mh. Mwandosya ambaye alishiriki katika kuanzisha mamlaka nchini alielezea chanzo cha Rais kuamua kuiweka EWURA kuwajibika Wizara ya Maji.

Alisema Sheria iliundwa kwa maana kwamba EWURA itatakiwa kupata ushauri kutoka katika sekta husika kwa maana ya masuala ya sera. Waziri hutoa miongozo ya kiutawala lakini mamlaka inajitegemea kiuamzi katika masuala ya udhibiti.

Akiunga mkono hoja hiyo, Bw. Masebu alisema mfumo uliopo umeonesha mafanikio mazuri na angeshauri utaratibu huo kuendelea.

Waziri wa Nishati na Madini, Mh. William Ngeleja alipongeza ufafanuzi wa Mh. Mwandosya.

Ukumbi wa Msekwa ulikuwa umejaa wabunge wenye shauku ya kujua shughuli za EWURA.

KAMPENI YA EWURA YA UHAMASISHAJI YAINGIA SONGEA NA TUNDURU KWA KISHINDO

Na Michael Mshighwa

JUKWAA kuu na mengine mawili ya Uwanja wa Michezo wa Kumbukumbu ya Majimaji mjini Songea yalijazwa na viongozi wa nyumba kumi na makatibu kata wa mji huo na vitongoji vyake, waliokusanyika kwa ajili ya kujifunza shughuli za EWURA, sekta za usimamizi na jinsi malalamiko yanavyopokewa na kushughulikiwa.

Tukio hilo lilibarikiwa na uwepo wa viongozi mashuhuri wa kisiasa na kiserikali kutoka ngazi mbalimbali za serikali za mitaa na serikali kuu. Miongoni mwao walikuwa ni Katibu Mkuu wa Chama Tawala (CCM), Mhe. Yusufu Makamba (Mb). Mhe. Dk. Diodurus Kamala (Mb), Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Mhe. Dk. Emmanuel Nchimbi (Mb) Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mhe. Dk. Christine Ishengoma, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma – miongoni mwao.

Tunduru mjini, ukumbi mashuhuri wa Skyway ulijaa zaidi ya washiriki 150 – wengi wao wakiwa ni viongozi wa wanawake kutoka Wilaya ya Tunduru. Kuwapo kwa Mhe. Injinia Stella Manyanya (Mb) na viongozi wengine wa vijana na kata ilikuwa ni ishara nzuri kwa kampeni hiyo ya EWURA wilayani humo.

Kifungu cha 6(e) cha Sheria ya EWURA namba 414, ya sheria za Tanzania, kinatamka kuwa moja ya wajibu wa EWURA ni kutoa maarifa kwa umma, ufahamu na kuelewa sekta zinazosimamiwa, ikiwa ni pamoja na haki na wajibu wa mlaji na mtoaji huduma, kuibuka kwa malalamiko na migogoro na jinsi ya kuyatatua na wajibu, majukumu na shughuli za Mamlaka.

Kwa mwaka wa fedha wa 2009/10, EWURA imetenga fedha kwa ajili ya kuelimisha umma juu ya shughuli zake. Uelimishaji umma Songea na Tunduru ilikuwa ni kazi ya kwanza ya mwaka huu wa fedha.

Kikundi cha watumishi wanne wa EWURA kikiongozwa na Mkurugenzi wa Umeme, Injinia Anastas P. Mbawala, kilikwenda Songea na Tunduru kuendesha mikutano ya uelimishaji umma kwa wadau.

Wengine katika kikundi hicho alikuwa ni Ofisa Mkuu wa Huduma kwa Mteja, Injinia Michael Mshighwa, Ofisa Huduma kwa Mteja, Bi Mariam Mmbaga na dereva wao Robert Nyirenda.
Katika mada yake, Injinia Mbawala alianza kwa kuelezea historia, sababu za kiuchumi jamii zilizosababisha mabadiliko ya bodi za usimamizi. Alisema haja ya kuwa na huduma bora, za uhakika na zinazokidhi mahitaji ni kigezo muhimu ambacho kinasababisha mgawanyo wa kazi za utungaji sera na sheria na majukumu ya usimamizi na ufuatiliaji.

Serikali inabaki kuwa na jukumu la kutunga sera na kutekeleza sheria wakati kazi ya usimamizi inaachwa kwa bodi za usimamizi. Injinia Mbawala aliiambia hadhira kuwa dira ya EWURA ni katika kutoa huduma bora, rahisi na endelevu za nishati na maji kwa wote. Alisema katika kuhakikisha kwamba dira hiyo inafikiwa; EWURA imejipangia mikakati ya kuhakikisha zinatolewa huduma bora za maji na nishati kwa kuzingatia kanuni za kimataifa na kuboresha ustawi wa jamii ya Tanzania.

Alisema katika umri wake wa miaka mitatu, EWURA imetoa mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa, hususan katika kuhakikisha kuwa soko si tu ni huru na la ushindani, lakini pia ni huru kwa kila mdau. Injinia Mbawala aliiambia hadhira hiyo juu ya kuwapo kwa kitengo cha kupokea malalamiko cha Ewura na kuwa walaji wako huru kuwasilisha malalamiko yao inapolazimika.

Baada ya hotuba iliyowasilishwa kwa umahiri mkubwa na Injinia Mbawala, washiriki waliibua masuala kadhaa wakitaka ufafanuzi kutoka EWURA. Walikuwa na hamu ya kujua sababu ya kubadilikabadilika kwa bei ya mafuta na kwa nini bei ya mafuta Tunduru imepanda kutoka Sh 750 hadi Sh 1,000 kwa lita katika kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

Eneo lingine ambako liliwasumbua ni takwimu kuhusu uchakachuaji wa mafuta na hatua zinazochukuliwa dhidi ya wakosaji. Washiriki walitaka kujua mikakati inayotumiwa na EWURA kupambana na uhalifu huu.

Watu wa Songea na Tunduru waliishukuru EWURA kwa kuwapa kipaumbele katika kampeni hiyo kwa mwaka huu wa fedha. Kikundi hicho kilipata pia fursa ya kutembelea vituo vya umeme vya Songea, Tunduru na Masasi ambako kilipewa maelezo kuhusu hali ya nishati hiyo katika eneo hilo.

MAREKEBISHO KATIKA KUINUA MAENDELEO YA MIRADI MIDOGO YA NISHATI TANZANIA

Na Mhandisi Norbert Kahyoza

SEKTA ya nishati ya umeme nchini Tanzania inahodhiwa na Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco). Hadi mwihoni mwa mwaka jana, uwezo wa uzalishaji nishati hiyo ilikuwa Megawati 1006.

Umeme utokanao na maji unachukua asilimia 55.7, huku kiasi kinachobaki kikitokana na nishati nyingine ambayo ni ya gesi na mafuta jamii ya petroli.

Kiasi hiki ambacho awali kilisaidiwa na megawati 185 kutokana na mitambo ya dharura, kilitoa umeme kwa walaji 740,954 wenye mita wanaokadiriwa kuwa asilimia 11 ya wanaotumia umeme nchini- ambapo dhana ya kuwa na umeme ni kuwa nao kwa matumizi ya majumbani. Mahitaji ya juu ya umeme yalikuwa ni megawati 690. Mapema mwaka 2006, Tanesco ililazimika kuanzisha mgawo wa umeme ili kukabiliana na upungufu wa nishati hiyo, ambapo pia ilifikia kukodi mitambo ya kufua umeme wa dharura.

Gridi ya Taifa inahudumia sehemu ndogo tu ya nchi, ikiacha maeneo mengi hususan mijini, yakitegemea mitambo inayotumia dizeli kufua umeme kwa huduma ambayo ni duni lakini pia yenye gharama kubwa (zaidi ya dola 20 za Marekani kwa kilowati) kiasi cha kuikamua Tanesco kutokana na mtazamo wa kuwa na viwango sare vya malipo ya bili.

Serikali ya Tanzania, baada ya kugundua kuwa utoaji usioridhisha wa umeme ni moja ya vikwazo vya maendeleo, iliamua kuja na sera muafaka ambazo zitahimiza maendeleo ya miradi midogo ya nishati asilia. Tasnia ya nishati hiyo ilionekana kuwa katika ngazi za mwanzo za maendeleo yasiyoratibiwa ipasavyo (Mathalan ukosefu wa sheria au miongozo).

Miradi michache iliyoanzishwa iliegemea zaidi katika mahitaji ya mfadhili wake kibiashara. Hivyo wahusika katika tasnia hii walikuwa wachache na zaidi walikuwa ni wa mashirika ya kidini na kwa kiasi fulani Tanesco yenyewe. Hakukuwa na wahamasishaji wa miradi ya kimikakati, wafadhili, kampuni za utoaji huduma au wapangaji mipango.

Kwa nini miradi midogo ya nishati asilia sasa?

Nishati asilia ni itokanayo na vyanzo asilia-kama vile mionzi ya jua, upepo, nguvu za maji, mawimbi, umeme wa gesi ya taka, nakadhalika, ambayo hupatikana kwa njia za asili. Zipo sababu na faida nyingi katika matumizi ya vyanzo hivi vya asilia katika viwango vidogo kwa sasa, lakini pia baadaye. Faida kubwa zinajadiliwa hapa chini.

Raslimali nyingi

Vyanzo vya nishati ya asili vinachangia chini ya asilimia moja ya mahitaji ya Taifa ya nishati; hata hivyo, utafiti mwingi umebaini mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na wa hivi karibuni uliouhusu umeme vijijini uliofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

- Uwezekano wa kuwa na vyanzo vingi unatahminiwa kama ifuatavyo: Uzalishaji mdogo wa umeme wa maji (chini ya megawati 10); inakadiriwa kuzalisha megawati 250 ambapo ni megawati 8 tu ndizo mpaka sasa zimeshavunwa.

Utafiti mwingi umefanyika katika miongo ya hivi karibuni, ukitoa mwelekeo katika upembuzi wa kiteknolojia.Utafiti ambao umejumuisha uchambuzi wa kiuchumi unaoonesha kuwapo kwa maeneo machache yanayoweza kuzalisha umeme kwa gharama za kiushindani kuliko mahitaji yake.

- Chanzo cha umeme wa upepo nacho kimetafitiwa na maeneo kadhaa kuonesha kuwa na upepo unaoweza kutumika kuzalisha nishati hiyo. Maeneo hayo ni Singida, Makambako, Dodoma, nk.

- Nishati ya jua nchini inakadiriwa kupatikana kwa wastani wa kutoa kilowati 5-5.6 za umeme kwa meta ya eneo kwa siku kwa mujibu wa ramani ya maeneo ya jua duniani. Hiki ni kiwango cha juu kabisa barani Afrika.

- Nishati asilia- inapatikana na kutumika sana nchini Tanzania. Inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 90 ya watumiaji nishati nchini Tanzania kutokana na nishati asilia ni wale wanaotumia kuni. Chanzo hiki cha nishati kinahusisha aina nyingi ya malighafi, kama vile gesi itokanayo na mabaki ya miwa, mabaki ya mbao, takataka za viwandani, majumbani nk. Gesi ya mabaki ya miwa pekee inakadiriwa kuzalisha hadi megawati 200 za umeme, wakati mabaki ya mbao yanaweza kuzalisha zaidi ya hapo.

Nishati safi
Vyanzo vya nishati asilia vinajulikana kwa kuwa rafiki wa mazingira (safi) na kuthibitishwa kuwa na athari nzuri kwa kuzingatia mabadiliko ya hali ya hewa.
Kuna msisitizo wa kimataifa kwa sasa wa upatikanaji wa nishati safi katika eneo hili la mafuta ya asili.

Ongezeko la uwezo kwenye gridi na gridi ndogo
Kutokana na wasiwasi uliopo juu ya mabadiliko ya hali ya hewa – ikijumuishwa na kupanda kwa bei ya mafuta na tishio la kushuka kwa akiba ya haidrokaboni- chanzo mbadala cha nishati kinahitajika kuongezwa kwenye uwezo wa Gridi ya Taifa.

Hatua hii itaweza angalau kukidhi mahitaji yanayoongezeka kila siku na pia kupunguza muda mrefu wa kuwa na miradi mikubwa ya nishati.

Miradi hiyo mikubwa inahitaji mtaji mkubwa na muda mrefu kukamilika, na jinsi mahitaji ya nishati yanavyoongezeka, ndivyo uwezo nao unavyopungua katika kukidhi mahitaji hayo.

Chachu ya umeme vijijini
Vyanzo vingi vya umeme asilia viko katika maeneo ya karibu na watu wa vijijini. Mkakati huu wa kuanzisha miradi midogo ya nishati itaongeza kiwango cha upatikanaji wa umeme huo katika maeneo hayo na hivyo kutoa fursa za ajira kwa watu wasio na elimu na walio na elimu kidogo.

Sera wezeshi
Serikali ya Tanzania inachukulia kukua kwa tasnia ya nishati asilia kama kipengee muhimu katika mkakati wa maendeleo ya sekta ya nishati vijijini. Sera nyingi na sheria zimepitishwa ili kuwezesha ukuaji wa tasnia hiyo. Nazo ni:

- Tamko la Sera ya UmemeVijijini, ambayo inataka kufikiriwa kwa miradi ya gharama nafuu – ikiwa ni pamoja na nishati asilia.
- Sheria ya Nishati Vijijini (2005) iliyoanzisha Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Mfuko wa Nishati Vijijini (REF) kwa kazi kubwa ya kupanga ruzuku kwa ajili ya nishati vijijini, ikiwa ni pamoja na mifumo ya nishati asilia;
- Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (Ewura) ambayo inampa mdhibiti wajibu wa kupanga bei, zikiwa ni pamoja na zinazohusu wazalishaji binafsi wa nishati asilia na kuwafikiria masikini ambao wanapatikana zaidi vijijini na katika viunga vya mijini; na,
- Sheria ya Umeme ya 2008 ambayo inatambua kuwapo kwa miradi midogo ya umeme (SPPs) kama vile jenereta zenye uwezo wa kuzalisha umeme wa kati ya kilowati 100 na megawati 10.

Pia, Sera ya Taifa ya Nishati (2003) inatamka haja ya kupunguza utegemezi katika mafuta kwa baadhi ya gridi na maeneo ya vijijini na kupendekeza utafiti zaidi na uendelezaji wa nishati asilia, hususan katika mikakati ya maendeleo ya umeme vijijini.
Pamoja na mambo mengine, sera inatamka kwamba “ipo haja ya kuanzishwa kwa mpango wa maendeleo ya nishati asilia na kuanzisha muundo wa kitaasisi na mbinu za kukabiliana na vikwazo vya kiteknolojia, kijamii na kifedha kwa ajili ya kueneza teknolojia ya nishati asilia.”

Utekelezaji wa sera
Tangu mwaka 2006, Wizara ya Nishati na Madini, ilizindua mipango ya kuzitekeleza sera hizi kupitia kuanzishwa kwa mipango ya kisheria na kiufundi ambayo inachangia maendeleo katika sekta binafsi ya SPPs katika misingi ya vyanzo vya nishati asilia.

Yafuatayo ni mambo ambayo yamefanikiwa.

- Taratibu za Makubaliano ya Ununuzi Mdogo wa Nishati na Bei kwa ajili ya watumiaji waliounganishwa na gridi na mifumo mingine inayojitegemea zimeshaidhinishwa na Ewura na zinatumika hivi sasa.
- Ewura inakamilisha maandalizi ya Miongozo na Kanuni kwa ajili ya utaratibu wa kuendeleza Miradi Midogo ya Umeme.
- Ewura inakamilisha uandaaji wa nyaraka za mfano zitakazotumika pamoja na miongozo hii. Hiyo ni pamoja na fomu za maombi, vigezo vya leseni, vibali, fomu za usajili, barua ya kusudio, nk.
- Kuanzishwa kwa Kikundikazi cha Maendeleo ya Umeme Mdogo (WGSPD) kitakachojumuisha taasisi muhimu ambazo ni wadau. WGSPD ina mamlaka ya kuhifadhi takwimu za SPP za kila mwaka na kuwasilisha Ewura bei zinazotumika kwa ajili ya kuidhinishwa.
- Hadi Januari 2009 takriban wadau 27 wa maendeleo walisajiliwa REA.
- Baada ya kuchapishwa kwa bei za SPPs zilizounganishwa katika gridi kuu na ndogo mwaka 2009 SPPAs tatu zitasainiwa kati ya wadau hao wa maendeleo na Tanesco.

MAADHIMISHO YA MIAKA MITATU YA EWURA

Na Mhandisi Charles Omujuni

ZIPO tarehe nyingi katika maisha ambazo mtu hupaswa kuzikumbuka. Fikiria siku yako ya kwanza shuleni. Sawa pia na siku yako ya kwanza katika ajira mpya. Siku hiyo utapaswa kujua ni wapi unaweza kupata huduma ya maji na chakula, ni mahali pageni kabisa kwako, wakati mwingine unakutana na watu wapya kabisa na utajiuliza nani ni nani?

Hakika, siku ya kwanza popote ni muhimu katika maisha ya binadamu. Usithubutu kabisa kuipuuza siku ya kwanza uwapo popote pale katika nafasi yoyote. Ijumaa siku ya kwanza ya Septemba mwaka 2006, wengi wetu tuliamka mapema asubuhi hiyo mwanana na kwenda katika sehemu yetu mpya iitwayo EWURA, katika ghorofa la Harbour View Towers. Hakuna aliyefika hapo baada ya saa 1.30 asubuhi siku hiyo.

Kila mmoja alijawa bashasha, akifungua ukurasa mpya katika maisha yake, akiwa na matumaini makubwa, na si sisi tu, lakini hata wenza wetu katika ndoa, watoto, jamaa na marafiki. Sisi waja wapya, kila mmoja alivalia nadhifu, alipokewa kwa unyenyekevu na sura iliyojawa na tabasamu ya Mkurugenzi Mkuu, Bw. Haruna Masebu 'HM', katika chumba cha mikutano.

HM, muasisi wa EWURA, alitoa hotuba ya ufunguzi huku akionekana kabisa kulemewa na furaha akifuta chozi la furaha, kwani ndoto yake ya muda mrefu sasa ilikuwa inatimia. Tulipiga picha ya pamoja ya kumbukumbu na mara kazi ikaanza.
Neno adhimu nililolinyakua kutoka hotuba yake ni KAIZEN, ambalo ni la kijapani likiwa na maana ya falsafa ya kazi, akihimiza haja ya kuwapo uboreshaji endelevu wa maarifa ya kila mmoja wetu. EWURA iliendelea kupata watumishi werevu na weledi na kuwaingiza katika ulimwengu wa utendaji kazi.

"Majaliwa yetu hayapaswi kuwa mikononi mwa nyota zao ila miongoni mwetu wenyewe," alisema Williams Shakespear. Katika kipindi chote cha miaka mitatu yamekuwapo matukio mbalimbali na masimulizi kadhaa. Nimepata bahati njema si kwa sababu ya kufanya kazi na watu wema tu, bali wenye nyoyo kuu.
Familia ya EWURA ni karimu, yenye kutia moyo lakini jambo kubwa ni inayozalisha na yenye watu wa ajabu ambao wanageuza nadharia kuwa vitendo. Sifa iliyoje! Wadhibiti wapya sehemu yoyote duniani, ikiwamo EWURA, kwa kawaida hukabiliana na "matatizo ya kuanza" katika siku zao za awali. Huchukua muda kubadili fikra na kuaminiwa na wadau. Marafiki wa zamani hukimbia, na kwa uhakika: " Kama mdhibiti anafanya kazi yake vizuri, anapoondoka kazini rafiki pekee anayesalia huwa ni mbwa wake," anasema Dk Bernard Tenenbaum ambaye ni Mdhibiti mzoefu, Mshauri katika Benki ya Dunia.
Anaongeza kuwa kama kinyume chake kinawezekana, basi kutakuwa na kitu ambacho hakiendi sawa katika mfumo wa udhibiti, hicho kitatakiwa kufanyiwa kazi mara moja.

Wafanyakazi wa EWURA wanatanguliza maslahi ya umma kuliko yao. Tunapambana na rushwa katika kila ngazi, na kwa uzalendo tunalinda mafanikio ya Tanzania.

"Tutakilinda kisiwa chetu, kwa gharama yoyote ile, tutapigana fukweni, tutapigana ardhini, tutapigana mashambani na mitaani, tutapigana vilimani, hatutasalimu amri kamwe!"-Sir Winston Churchill.
Hivyo kwa kuhitimisha, nataka kuipongeza familia ya Ewura kwa kuonesha utendaji mzuri wa udhibiti katika kipindi hicho cha miaka mitatu iliyopita. ALUTA CONTINUA!

Wafanyakazi waanzilishi wa EWURA wakiwa katika picha ya pamoja mwaka 2006.